F2 ENDYEAR ASSIGNMENT

KISWAHILI

10+ HOLIDAY ASSESMENTPAPERS

Dear Students, Make Maximum Utilization of limited time Available to Attempt and Work on these Year-Round Examination Trials.

A Comprehensive Evaluation Analysis of F1 & F2 Syllabus Coverage.

SERIES 1

For Marking Schemes

Call/WhatsApp 0746 222 000

MWALIMU CONSULTANCY

FORM 2 EXAMINATION TRIALS

KISWAHILI

PRACTICE TEST 1

TIME: 2 HOURS

NAME…….. ADM NO……....

SIGN……..……. DATE;…….....

Answer All the questions in the spaces provided

1. UFAHAMU (Alama10)

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali

Tokea muundo mpya wa serikali ya ugatuzi uanze kutekelezwa miaka miwili iliyopita, kumeendelea kushuhudiwa matatizo mengi hali iliyopelekea kushuhudiwa kwamsururu wa migomo na maandamano ya raia. Fujo za karibuni kabisa ni zile zinazoshuhudiwa katika miji mikubwa za wachuuzi na wafanyibiashara wakipinga hatua za serikali za kaunti kuwatoza ushuru takribani kwa kila huduma na bidhaa ikiwemo wanyama, kuku na ndege. La kuhuzunisha zaidi katika baadhi ya majimbo imeripotiwa kuwa raia wamelazimishwa kulipa ushuru kwa kutaka tu kuona maiti za jamaa zao kwenye vyumba vya kuhifadhi maiti.

Wanasiasa wameonekana kuwa na wakati mgumu kutetea mfumo huu mpya wa ugatuzi huku baadhi wakisema kwamba matatizo yanayoshuhudiwa kwa sasa yametokana na ugeni wa mfumo huo. Wengine wameinyoshea kidole serikali ya kitaifa kwamba ndiyo inayosambaratisha muundo huu. Wengine wanahoji kuwa bado ni mapema na kwamba kunatajika muda mrefu ili kufaulu.

Ni wazi kwamba kumekosekana nidhamu bora ya kusimamia maisha ya raia nchini Kenya. Matatizo yanayokumba raia kwa sasa ni dalili kuwa mfumo wa serikali ya ugatuzi umeongezea chumvi kwenye kidonda badala ya kutibu. Swali ni je, hadi lini nidhamu ya kusimamia raia itakuwa ni suala la majaribio na makosa?

Hatua ya kuwarundikizia raia ushuru mkubwa ni kitendo cha unyonyaji na cha dhuluma kinachofaa kupingwa. La kufahamishiwa hapa ni kwamba ushuru ndio njia kubwa ya kuzalisha mapato ya serikali zinazojifunga na mfumo wa kimagharibi wa kiuchumi wa kibepari ikiwemo Kenya. Asilimia 90 ya mapato ya serikali za kibepari huegemea ushuru. Kwa hivyo hatua ya serikali za kaunti katika kuwanyonya raia kwa kuwalipisha ushuru si ajabu bali ni thibitisho kuwa jamii ya Kenya inaongozwa na nidhamu ya kiuchumi ya ubepari mfumo wa unyonyaji na ukandamizaji. Ukweli

unabakia kuwa ndani ya serikali za kibepari raia ndio hubebeshwa mzigo wa ushuru unaoishia matumboni mwa viongozi!

Miito ya mabadiliko ya katiba na ya miundo mipya ya kiutawala si lolote ila ni moja tu ya hatua za mfumo wa kibepari kujipa muda wakuishi na kuziba aibu zake za kushindwa kusimamia maisha ya watu. Kufeli huku kwa mfumo huu kunashuhudiwa hadi kwenye nchi kubwa za kibepari kama Marekani na Uingereza hivyo nazo zimekumbwa tele na maandamano na fujo za raia wakilalamikia hali ngumu ya maisha.

Maswali

a) Yape makala haya anwani mwafaka. **(alama 1)**

……

b) Eleza mtazamo wa wanasiasa kuhusu utepetevu wa mfumo huu. **(alama 3)**

……

……

……

c) Migomo ni zao la matatizo yaliyogatuliwa kutoka kuu. Toa sababu nyingine zinazosababisha migomo katika serikali za ugatuzi **(alama 3)**

……

……

……

d) Thibitisha jinsi mfumo wa ugatuzi umeongeza chumvi kwenye kidonda badala ya kutibu **(alama 2)**

……

……

e) Eleza maana ya neno lifuatalo **(alama 1)**

i) Ugatuzi

2. MATUMIZI YA LUGHA

a) Tofautisha kati ya mofimu huru na mofimu funge. **(Alama 2)**

……

……

……

b) Ainisha mofimu hizi. **(Alama 2)**

i) Mende

ii) Mpwa

c) Ainisha viambishi viambishi katika neon lifuatalo**.** **(Alama 2)**

Anayemtembelea

d)Tunga sentensi moja ili kutofautisha maana. **(Alama 2)**

i) Baba

ii) Papa

e) Tumia neno safi kama nomino kutungia sentensi. **(Alam 2)**

……

……

f) Tumia kivumishi kiashiria cha mbali kidogo pamoja na ngeli ya I- ZI katika sentensi sahihi.

(Alama 2)

……

……

……

g) Kanusha katika ukubwa wingi. **(Alama 2)**

Mtoto alikuwa amelia.

……

ISIMU JAMII

h. Taja sifa tano za sajili ya hotelini. **(Alama 5)**

CHETI CHA KUHITIMU ELIMU YA SEKONDARI TATHMINI YA PAMOJA

……

……

……

……

……

……

……

……

FORM 2 EXAMINATION TRIALS

KISWAHILI

PRACTICE TEST 2

TIME: 2 HOURS

NAME…….. ADM NO……....

SIGN……..……. DATE;…….....

Answer All the questions in the spaces provided

SEHEMU A: INSHA (ALAMA 20)

Andika insha ifuatayo kwa kutumia maneno yasiyopungua 300

Wewe ni mkurugenzi wa elimu katika kaunti yako. Umealikwa katika kongamano la wanafunzi linalohusiana na tatito la upataji mimba baina ya wanafunzi katika shule za msingi na sekondari. Andika hotuba yako kwa wanafunzi hao huku ukieleza sababu zinazosababisha tatito hilo na jinsi ya kulitatua.

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

SEHEMU B: UFAHAMU (ALAMA 15)

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali

Idara ya polisi nchini imelaumiwa kwa muda mrefu kutokana na visa vya mauaji ya kiholela, utepetevu na ufisadi miongoni mwao. Ni kutokana na kilio cha mwananchi pamoja na mashirika yasiyo ya kiserikali ambapo serikali imejitolea sabili kubadili hali katika idara hiyo huku tume mbali mbali zilizobuniwa zikitoa mapendekezo muhimu ya kurekebisha ishara hiyo. Matokeo ya hivi punde kutoka kwa shirika la 'Transparency International' liliorodhesha idara ya polisi kama idara fisadi zaidi nchini, maoni ambayo yalisisitizwa na shirika la kutetea haki za kibinadamu. Ufisadi bado umekita mizizi katika idara ya polisi kama idara fisadi zaidi nchini, maoni ambayo yalisisitizwa na shirika la kutetea haki za kibinadamu. Ufisadi bado umekita mizizi katika idara ya polisi tangu mabadiliko yaanze upande wa trafiki na hata ndani ya polisi.

Serikali imejitolea kupambana na ufisadi unaoonekana kuwa kidonda ndugu katika idara ya polisi. Wananchi wanasema kuwa polisi ni mafisadi na kusahau kuwa ufidisadi unashirikisha watu wawili na wote wanapaswa kufunguliwa mashtaka. Ili kuleta mabadiliko muhimu katika idara ya polisi, mapendekezo yote pamoja naya tume zingine za hapo awali lazima yatekelezwe kwa mujibu wa katiba mpya. Lazima mabadiliko yaanzie juu kwani maafisa wadogo hulazimishwa kuchukua hongo ili wapelekee wakubwa wao. Ni lazima shughuli ya kuwachagua maafisa walio bora ifanyike kisheria ili mabadiliko yaanze kutoka kwa wakuu na maafisa wa polisi.

Polisi kidogo wameweza kubadili ile lugha yao ya matusi na ukali kwa raia. Raia naohawajabadilika. Wengi wao bado huwaogopa polisi na itachukua muda kwani wanadhania kuwa kikosi ni kile kile cha kitambo. Kwa upande wa polisi, hakuna mageuzi yamefanyika. Unaposafiri kuja mjini, polisi wangali wanachukua hongo kutoka kwa wenye matatu na kuwaruhusu kubeba kupita kiasi pia usalama umedorora sana kwani kumekuwa na visa vingi vya mauaji hapa mjini. Ukiangalia maafisa wa polisi, hakuna mageuzi makubwa yameshuhudiwa haswa kwa upande wa polisi, hakuna mageuzi makubwa yameshuhudiwa haswa kwa upande wa maafisa wa trafiki. Bado ni wale wale na ufisadi ungali upo.

Mabadiliko ambayo tunataka ni kuwa polisi wasikae mahali kwa muda hadi wanajuana na mafisadi na majambazi. Maafisa wa polisi wanafaa kuhudumu katika kituo kimoja kwa muda usiozidi miaka mitatu. Kwa kufuata njia hiyo mabadiliko yatapatikana. Juhudi nyingi zikielekezwa katika kubadili kikosi cha polisi wananchi wanapaswa kuhamasishwa ili nao waweze kubadilika haswa kuhusiana na mtazamo wao kwa maafisa wa polisi. Huku tukijaribu kubadili maafisa wa polisi, wananchi pia wanapaswa kuelimishwa ili waweze kubadili mtazamo wao kuhusu maafisa hao. Ni bayana kuwa ili kuweza kuleta mabadiliko ya kutamanika katika kikosi cha polisi na haswa katika kupambana na ufisadi uliokita mizizi wananchi sawia na maafisa wa polisi wana jukumu la pamoja kuleta mabadiliko hayo yatakayopelekea kuwepo kwa mlahaja mzuri kati ya maafisa wa polisi na raia. Hatimaye, kuwepo kwa huduma bora itakayochangia pakubwa kuboresha uchumi wa taifa na kuafikiwa kwa ruwaza ya mwaka 2030.

Maswali

a) Kipe kifungu hiki kichwa mwafaka **(alama 1)**

……

b) Thibitisha kuwa ufisadi ni kidonda ndugu ukirejelea makala haya **(alama 2)**

……

……

……

c) Ni vipi ufisadi katika idara ya polisi unaweza kuzikwa katika kaburi la sahau? **(alama 2)**

……

……

……

d) Wananchi ndio wanapaswa kulaumiwa kwa ufisadi. Thibitisha **(alama 2)**

……

……

……

e) 'Serikali imepiga hatua katika kuleta mabadiliko katika idara ya polisi'. Onyesha kinyume cha usemi huu. **(alama 2)**

……

……

……

f) Taja manufaa yoyote mawili yanayotokana na mabadiliko katika idara ya polisi **(alama 2)**

……

……

……

g) Eleza maana ya; **(alama 4)**

i) Mlahaka

……

……

ii) Utepetevu

……

……

iii) Kujitolea sabili

……

……

iv) Hongo

……

……

SEHEMU C – MATUMIZI YA LUGHA

a) i) Taja sauti zozote mbili zinazotamkiwa kwenye kaakaa gumu **(alama 2)**

……

……

……

ii) Huku ukitolea mfano, eleza aina mbili za miundo ya silabi katika Kiswahili **(alama 2)**

……

……

……

b) Weka maneno yafuatayo katika ngeli zifaazo: **(alama 2)**

1. Ukuta ……
2. Kibogoyo ……..

c) Tunga sentensi ukitumia aina ya nomino zifuatazo;

i) Dhahania **(alama 1)**

……

……

ii) Za wingi **(alama 1)**

……

……

d) Tumia neno vibaya kama: **(alama 3)**

i) Kivumishi

……

……

ii) Kielezi

……

……

iii) Kiwakilishi

……

……

e) Ainisha vitenzi katika sentensi ifuatayo: **(alama 2)**

Juma alikuwa akienda kulima

……

……

……

……

……

……

f) Andika kwa hali timilifu **(alama 2)**

Mwalimu alikuwa hapa tangu asubuhi

……

……

……

g) Ainisha maneno katika sentensi ifuatayo:

Ala! yeye ni kiongozi mkuu mjini? **(alama 3)**

……

……

……

……

h) Onyesha viambishi awali na viambishi tamati katika neno lifuatalo: **(alama 2)**

Walichotupigia

……

……

……

i) Akifisha **(alama 3)**

mama aliwauliza nyinyi ndio mlituletea sahani vijoki na sufuria

……

……

……

j) Andika kwa wingi **(alama 2)**

Kibogoyo huyu ndiye aliyenipatia jiko hili.

……

……

……

k) Kanusha **(alama 2)**

Akiingia atamnunulia samaki wengi

……

……

l) Andika kinyume cha sentensi ifuatayo **(alama 3)**

Mahindi ya mama yamekua kwa kupata mvua ya kutosha

……

……

m) Andika udogo wa sentensi ifuatayo: **(alama 2)**

Mbwa aliyemwuuma mtoto ameuawa

……

……

n) Kamilisha sentensi zifuatazo kwa kutumia vitenzi na kauli zilizo mabanoni: **(alama 2)**

i) Kaka alim……dadake (Kimbia-tendesha) **(alama 1)**

ii) Pesa alizo ……..hazikutosha (leta-tendewa) **(alama 1)**

o) Andika msemo mwingine wenye maana sawa na ‘piga maji’ **(alama 2)**

……

……

……

SHEMU D – ISIMU JAMII

i) Eleza sababu mbili ambazo zinaweza kufanya lugha kufa/kufifia **(alama 2)**

……

……

……

……

ii) Taja sifa zozote nne za sajili ya siasa **(alama 8)**

……

……

……

……

……

……

……

……

……

SEHEMU E –FASIHI SIMULIZI

a) i) Taja majukumu yoyote matano ya fasihi simulizi **(alama 5)**

……

……

……

……

……

ii) Fasihi simulizi huendelezwaje leo? Taja namna tatu **(alama 3)**

……

……

……

b) Eleza maana ya dhana zifuatazo katika fasihi simulizi **(alama 8)**

i) Ulumbi

……

……

ii) Ngomezi

……

……

iii) Lakabu

……

……

iv) Misimu

……

……

c) Taja sifa zozote nne za mlumbi **(alama 4)**

……

……

……

……

……

FORM 2 EXAMINATION TRIALS

KISWAHILI

PRACTICE TEST 3

TIME: 2 HOURS

NAME…….. ADM NO……....

SIGN……..……. DATE;…….....

Answer All the questions in the spaces provided

FUNGUA SESAME

Jina la Nimrod lilipotea mara tu alipoanza kufanya kazi jijini Nirobi. Marafiki na jamaa zake waliamini kuwa alikuwa ameajiriwa huko mjini ingawa hakuna aliyeijua kazi yenyewe vizuri. Hata hivyo waliamini kuwa lazima alikuwa na *kibonge cha kazi* kwa sababu alivalia kinadhifu na kuishi maisha ya starehe. Tena yeye mwenyewe alikazania kusema kuwa amejiriwa kazi ya maana. Marafiki zake walimfahamu kama "Bwana Sesame". Mtu wa kwanza aliyempa jina hilo alisema alipendezwa na ujuzi na maarifa yake. "huyu hakosi ufumbuzi wa tatizo loote. Ni kama ule mlango wa kisa cha Ali Baba na *Wezi arobaini*. Ukisema 'fungua Sesame' unafunguka tu," alisema mtu huyo.

Jamaa walioishi naye katika mtaa wa urumo walishangazwa na utaratibu wake wa kazi. Mchana kutwa alishinda chumbani mwake. Mara nyingi utamkuta *ametulia tuli* akitazama *runinga* yake ndogo. Wakati mwingine atakuwa akifanya kazi yake ndogo ndogo huku *akipiga mluzi* bubu, ambao haukusikika vizuri. Wakati mwingine atakuwa akiusikiliza muziki kwenye chombo chake cha muziki kilichotingisha jingo zima kutokana na sauti yake nene.

Kwa kawaida alitoka chumbani jioni. Waliomjua walimchangamkia kutokana na uchangamfu wake. Alipenda sana mizaha. Waliopenda *kupiga soga* walivutiwa na maongezi yake hasa kuhusiana na magari. Aliyajua magari mengi. Mimi naweza kuijua aina ya gari kwa kuusikiliza mlio wake tu", alisema kila wakati. "wacha *kutuvungavunga* Bwana wee, haiwezekani !" atasema mwingine. "nini? Unajua mimi ndiye Bwana Sesame mwenyewe!" atasema, halafu wote *wataangua kicheko*.

Ilifika wakati kampuni kadha zilipoamua kuwapunguza wafanyakazi wake kutokana na hali mbaya ya kiuchumi. Lakini Bwana Sesame hakuwa mmoja wa hao. Hali yake ilibakia vile vile. Aliendelea kuvalia kinadhifu na kuishi maisha yake ya *fawaishi*. Wakati wenzake wanalalamikia hali ngumu ya maisha, Bwana Sesame hakuwa na lolote la kumsumbua. Aliendelea kukaa bila kazi

wala bazi. Lakini watu walitambua kuwa alikua na mazoea ya kutoka chumbani majira ya jioni. Hakuna aliyejua alirejea lini.

Siku moja Bwana Sesame alitoka jioni kama kawaida na kuelekea kwenye shughuli zake za kawaida. Siku hiyo jamaa mmoja wa mtaani alikumbana naye kwenye langu kuu. "Bwana Sesame, leo wapi yahe? alimwuliza. Bwana Sesame alimwangalia na kusema, "natoka nje kidogo yahe. Jiji hili lataka ustaarabu,' alijibu. Yule jamaa alimwangalia na kumwabia na kumwambia, "nina shida kidogo, sijui kama utanifaa mwenzangu. Wajua tena hali zenyewe siku hizi," alisema. Nini tena?' aliuliza Bwana Sesame.

"nina gari langu ambalo halina redio. Natafuta moja ya bei nafuu…. Kitu kama *sony* hivi," alisema. Bwana Sesame alimwangalia na kusema, "hiyo kazi nyepesi kwangu yahe, papai kwa kijiko!" alisema Bwana Sesame alicheka. Jamaa Yule alishukuru na wakaagana.

Bwana Sesame alishika njia kuelekea sehemu zake za kawaida majira kama haya. Naye Yule jamaa akapinda kama anaangalia mtaani, lakini baada ya muda akageuka na kuamua kumfuata Bwana Sesame.

Bwana Sesame *alishika tariki* mpaka sehemu ya mazoeea. Yule jamaa alimfuata kwa mbali na mwendo wa paka. Alimwona Bwana Sesame akiingia mahali palipokuwa na banda kuukuu. Muda si muda alitoka na jamaa wengine wakiwa wamevalia maguo ya ajabu. Yule jamaa aliwafuata hadi mahali palipokuwa na ujia mwembamba ulioachana na barabara kuu. Alijificha mahali, na kutokana na hali ya sehemu ile akawa haonekani.

Muda si muda palitokeza gari dogo lililokuwa likiendeshwa na mwanamke mmoja. Bwana Sesame na wenzake walitokeza na kutupa gogo lililomzuia Yule mwanamke.

Ghafla bin vuu walimvamia; wakaifungua milango ya gari mbio na kujivurumisha ndani. Gari lilitimuliwa kama risasi kuelekea upande wa pili. Wakati huo Yule jamaa ashaliangalia gari lenyewe na kuzihifadhi nambari zake. *Alishika njia* kurudi zake chumbani.

Siku iliyofuata huyo jamaa hakuwa kazini. Alipokuwa akifungua kinywa alisikia sauti ya kugongwa kwa mlango. Aliinika na kwenda kuufungua. Bwana Sesame aliingia ndani. "vipi yahe? Kujenda kazini leo? Au umelala sana Bwana?' alisema Bwana Sesame kwa uchangamfu wake. Muda si muda alimwonyesyesha redio ya gari aliyokuwa nayo. "umeipata mara moja hii kumbe?' aliuliza Yule jamaa. "si nilikwambia yahe! Mimi ndiye Bwana Sesame mwenyewe. Hii kwangu si kazi. Ninafahamiana na jamaa wengi wanaoifanya kazi hii," alisema Bwana Sesame. "naona kweli. Ehh Bwana we! Ndipo waswahili wakasema, *ukitaka kuvua vua na wavuvi*! Alisema Yule jamaa. "ni kweli kabisa!'" alijibu Bwana Sesame huku akicheka kwa furaha.

Yule jamaa alisimama kuelekea chumbani. Bwana Sesame alitulia akisubiri kupokea ujira wake. Muda mfupiulipita, kisha mlango wa nyumba ukagongwa. (yahe Bwana, kunagogwa huku!" Bwana Sesame akasema. Yule jamaa alitoka chumbani na kuelekea mlangoni. Mlango ulipofunguliwa waliingia waliingia askari polisi wawili. Bwana Sesame hakuwa na *upenyu* wa kutokea. *Alitiwa mikononi.* Hakujua kumbe Yule jamaa alikuwa kachero. Hapakuwa na ujanja tena. Siku hiyo *pwagu alipata pwaguzi*. Fungua Sesame haikufaa tena.

MASWALI

a) Kwa nini Nimrode alibatizwa ‘Bwana Sesame’**?** **(al 1)**

……

……

b) Kwa nini watu walioishi mtaani Urumo walishangazwa na utaratibu wa kazi wa Bwana Sesame? **(al 2)**

……

……

……

c) Unafikiria ni kwa nini Bwana Sesame alifahamu sana juu ya magari**?** **(al 1)**

……

……

d) Je, unafikiri yule jamaaa aliyaagiza aletewe radio alikuwa na haja sana na kifaa hicho kama alivyosema? **(al 2)**

……

……

……

e) Bwana Sesame alikuwa kachero. Unakubali? Toa maelezo? **(al 2)**

……

……

……

f) Yule jamaa alipoingia chumbani na kumwanch Bwana Sesame sebuleni unafikiri alikwenda kufanya nini? **(al 2)**

……

……

……

g) Je, hadithi hii ina mafunzo gani kwako? **(al 2)**

……

……

……

h) Eleza maana yamisemo ifuaayo kisha aitumie katika sentensi **(al 3)**

a. Piga mluzi
b. Piga soga
c. Shika tariki

3. Matumizi ya lugha **(al20)**

a) (i) Taja ala sogezi mbili za kutamkia **(al2)**

……

……

……

(ii) Tambua sauti yenye sifa zifuatazo **(al 1)**

konsonanti, kipasuo, ghuna, sauti ya mdomo

……

b) Tunga sentensi moja na uonyeshe nomino dhahania **(al 2)**

……

……

c) Tambua aina za maneno zilizopigiwa mistari

Mwanafunzi <u>mrefu</u> alienda <u>Nairobi</u> **(al1)**

……

……

d) Bainisha ngeli ya nomino iliyopiwa mistari. **(al 1)**

Jeshi la Kenya lilihamisha kifaru hadi mbuga ya masai mara.

……

……

e) Taja aina mbili za mofimu. **(al 2)**

……

……

……

f) Taja dhana zinazowakilishwa kisarufi na viambishi vilivyopigwa mistari **(al 1)**

Walituchezea

……

……

g) Bainisha kivumishi katika sentensi hii **(al 2)**

Matunda mawili yaliuzwa

……

……

h) Tunga sentensi ili kubainisha tofauti za kimaana kati ya maneno haya udogo na udongo **(al2)**

……

……

i) Kwa kutumia sentensi moja onyesha vitenzi sambamba **(al 2)**

……

……

j) Tunga sentensi moja na uonyeshe kiwakilishi kimilikishi **(al 2)**

……

……

ISIMU JAMII

a) Eleza maana ya istihali zifuatazo za isimujamii **(al 2)**

I. Isimu jamii

……

……

II. Sajili

……

……

b) Matumizi ya lugha hutegemea mambo kadhaa. Yaeleze yoyote manne **(al 8)**

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

FASIHI (AL 10)

Soma shairi hili kisha ujibu maswali yanayofuatia

Malenga mlotukuka, kwa tungo zenu teule
Tungo zenye kusifika, zenye na nasaha tele
Naomba la uhakika, jawabu enyi wavyele
Wa kuume tangu lini, kuukata wa kushoto!

Tangu dahari miaka, mikono ina upole
Meungana pasi shaka, ni miwili vile vile
Mmoja ukisumbuka, mwingine hujaa ndwele
Wa kuuma tangu lini, kuukata wa kushoto!

MASWALI

iv) a. Shairi hili ni la arudhi. Dhibitisha kwa kutoa sababu tatu **(al 3)**

……

……

……

b. Nakili kibwagizo cha shairi hili **(al 1)**

……

……

c. Eleza ujumbe mmoja unaojitokeza kwenye shairi **(al 2)**

……

……

……

v) a. Taja aina zozote mbili za hadithi **(al 2)**

……

……

……

b. "nikitembea yuko, nikikimbia yuko, nikiingia ndani hayuko

tambua kipera hiki **(al 1)**

……

……

taja dhima moja ya kipera hiki kijumla **(al 1)**

……

……

FORM 2 EXAMINATION TRIALS

KISWAHILI

PRACTICE TEST 4

TIME: 2 HOURS

NAME…….. ADM NO……....

SIGN……..……. DATE;…….....

Answer All the questions in the spaces provided

a) INSHA – ALAMA 20

"Wewe ni mwalimu mkuu wa shule yako. Andika hotuba utakayoitoa siku ya wazazi shuleni mwako."

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

UFAHAMU

Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali uliyoulizwa. **(ala 15)**

Mateso ya wanawakiwa ni suala la kijamii linalofaa kutazamwa kwa darubini kali. Hata hivyo wanoathirika zaidi ni watoto ambao bado wako katika umri unaohitaji kulelewa na kupewa mahitaji ya msingi kama mavazi, malazi, elimu na mengine anuwai. Hali ya kuachwa na wazazi imekuwa ikizikumba jamii tangu enzi za mababu na kila itokeapo, wanajamii huipokea kwa mitazamo tofautitofauti, hivyo kuwafanya wanawakiwa kuathirika sana.

Baadhi ya jamii zina imani za kijadi pamwe na mila zilizochakaa zinazozifanya kuamini kuwa baadhi ya vifo hutokana na laana. Wengine huchukulia kuwa mwendazake ameondolewa na ulogi. Imani kama hizi huifanya jamii kuwatia watoto waliochwa katika mkumbo ule ule, hivyo kuwaangalia kwa macho yasiyo ya kawaida. Hii husababisha dhana gande. Hali hii husababisha kuwachukulia watoto kama wanaotoka katika kizazi kilicholaaniwa. Jamii basi hukosa kuwapa watoto hawa stahiki yao. Hata wanapojitahidi kuiwania nafasi yao, waliowazunguka huwavunja mioyo. Jitihada zao huishia kuwa si chochote kwa kuwa jamii inawatazama kama waliolaaniwa.

Punde baada ya mzazi mmoja au wote wawili waendapo wasikorudi, inatarajiwa kwamba aliyeachiwa mtoto awe mzazi wake, mwanafamilia au jirani awajibike na kumtunza mwanamkiwa. Kunao kadha wa kadha wanaowajibika – nina wavulia kofia. Hata hivyo wengi hutelekeza jukumu hii walilopewa na Muumba. Si ajabu basi kuona kuwa idadi ya watoto wanaozurura mitaani inazidi kuongezeka kila uchao. Ukichunguza utakuta kuwa wengi wa watoto hawa ni waliopotelewa na wazazi wao. **Inakera** zaidi kugundua kuwa baadhi ya watoto hawa wana mzazi mmoja. Kwamba mke au mume wa mtu ameaga, au iwe kwamba mzazi mmoja alimza mtoto na kumwachia mwenzake mzigo wa ulezi, aliyeachiwa na jukumu la kumpa mwanawe mahitaji ya msingi. Machoni pa jalali, kila anayeupuuza wajibu huu ana hukumu yake siku ya kiama!

Ni haki ya kila mtoto kupata elimu. Katika katiba ya Kenya mathalan, elimu ya msingi, yaani kuanzia shule ya chekechea hadi kidato cha nne ni ya lazima. Tangu hapo hata hivyo, jamii zimekuwa zikiwanyima wanawakiwa wengi elimu. Kwamba kunao wachache wanaowaelimisha baadhi ya wanawakiwa ni kweli. Hata hivyo, wengine hukosa hata wa kuwapeleka katika shule ya chekechea, hivyo kuishia kutojua hata kuandika majina yao. Mfikirie mtu katika karne ya 21 asiyejua kusoma wala kuandika! Nani ajuaye, huenda huyo mwanamkiwa asiyepelekwa shuleni ndiye angalikuwa profesa, daktari, mwalimu, rubani au msomi mtajika na mtaalamu wa uwanja muhimu katika jamii!

Kila mtoto ana haki ya kulelewa hadi kufikia utu uzima kabla ya kupewa majukumu mazito. Katika katiba ya Kenya, utu uzima, ulio umri wa kuanza kufanya kazi huanzia miaka 18. Wanaohakikisha watoto hawa wametimiza utu uzima kabla ya kufanyizwa gange ngumu wanafaa pongezi. Hata hivyo wanawakiwa wamekuwa wakitumiwa na wengi kama punda wa huduma. Wanaaila wengine huwachukua wanawakiwa kwa machozi mengi wazazi wao waagapo na kuapa kuwahifadhi na kuwatunza wana wale wa ndugu zao, kumbe ni machozi ya simba kumlilia swara! Hata kabla ya mwili wa mzazi mhusika kuliwa na viwavi, mateso kwa mtoto yule huanza, akawa ndiye afanyaye kazi zote ngumu. Utakuta watoto wao wamekaa kama sultan bin jerehe huku mwanamkiwa yule akiwapikia, kuwafulia nguo, kudeki, karibu hata wa waoshe miili! Kazi kama zile za shokoa huwa za sulubu na aghalabu husindikizwa kwa matusi yasiyoandikika.

Baadhi ya **waja** walionyimwa huruma huwahadaa wanawakiwa na kuwapeleka ng'ambo wakitumia vyambo, kuwa wakifika kule watapata kazi za kifahari. Maskini wale huishia kushikwa shokoa, wakawa watumwa katika nyumba za waajiri wao, bila namna ya kujinasua. Wengine huishia kutumiwa kama watumwa wa 'Kimapenzi' katika madanguro, miili yao ikawa ya kuuziwa makahaba waroho wasiojali utu. **Kujinasua** kule huwa sawa na kujitahidi kuokoa ukuni uliokwishageuka jivu, maadamu wanawakiwa aghalabu hukosa watu wenye mioyo ya huruma ya kuwashughulikia. Wengi huitumia methali ' mwana wa ndugu kirugu mjukuu mwanangwa' kuwapuuzilia mbali wanawakiwa ambao hukimbiliwa tu wabinafsi hawa wanapofaidika wenyewe.

i) Kipe kifungu hiki kichwa mwafaka. **(ala.1)**

……

……

ii) Eleza dhana ya 'Mwanamkiwa. **(ala. 1)**

……

……

iii) Ni kategoria gani ya wanawakiwa inayosumbuka sana? **(ala. 2)**

……

……

iv) Taja mambo mawili ambayo baadhi ya imani na mila za jadi huchukulia kuwa chanzo cha uanaukiwa. **(ala.1)**

……

……

v) Eleza kwa kifupi hali ya elimu ya wanawakiwa. **(ala.2)**

……

……

vi) Taja mateso mawili ambayo wanawakiwa wanaoahidiwa kulepekwa ng'ambo hukumbana nayo. **(ala.2)**

……

……

vii) Eleza unafiki wa baadhi ya watu wa jamii ya wanawakiwa. **(ala.3)**

……

……

……

viii) Eleza maana za maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika makala. **(ala.3)**

Inakela

Waja

Kujinasua

UFUPISHO

<u>Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali uliyoulizwa</u>

Wanawake wanaoishi katika maeneo ya mashambani katika nchi zinazoendelea ni baadhi ya watu waliotopea na kubobea kwenye umaskini mkubwa na wanaoathiriwa na matatizo kwa kiwango kikubwa ulimwenguni. Jumla ya idadi ya wanawake hawa wanaoishi chini ya kiwango cha chini cha umaskini inakadiriwa kuwa zaidi ya milioni 600. Hii ni idadi kubwa hasa ikikumbukwa kuwa ni asilimia kubwa ya wanawake wanaoishi kwenye maeneo haya.

Ulimwengu umeshuhudia ongezeko la idadi ya watu au dadiwakazi; kuwako kwa matatizo ya kiuchumi ulimwenguni; mitafaruku na vita vya kikabila, majanga ya kiasilia kama mafuriko ya maji, ukame au milipuko ya volkeno katika maeneo yanayoathiriwa nayo. Sababu nyingine ni uharibifu na ushukaji wa hali ya kimazingira, mabadiliko ya desturi au thamani za kitamaduni; kusambaratika kwa familia au misingi ya familia; utengano na hasa wakati wa shida pamoja na uhamaji wa wanaume na kuwaachia jukumu kubwa. Aidha kuna kuongezeka kwa hali ya wanawake kuwa wazazi pekee na hivyo kuongeza idadi ya miji inayoongozwa na wanawake na kukosekana kwa mikakati bora au ifaayo ya kupambana na maisha.

Wanawake wanaoishi mashambani wanaathrika vibaya sana. Kwanza, kama masikini wanaishi katika mazingira makali. Pili, kama wanawake wanakabiliana na mapendeleo ya kisera na kitamaduni ambayo yanaudharau na kuupuuza mchango wao katika maendeleo. Tatu, kama viongozi wa miji (hasa wale wanaolea na kuzitunza jamaa zao peke yao) wanalazimika kupambana na uongozi wa miji pamoja uzalishaji. Aghalabu hawapati usaidizi au auni yoyote katika majukumu kama haya: wanalazimika kupambana nayo peke yao. Katika hali zote tatu zilizotangulia, wanawake hawapati nafasi zifaazo kushiriki katika maamuzi ya masuala yanayowahusu. Masuala mengi yanaamuliwa na wanaume bila ya kuwahusisha.

Licha ya dhiki yao kubwa, wanawake hawa wanachangia katika maendeleo ya kijamii na kiuchumi kwa njia tatu kuu. Mchango huu unaonekana katika kiwango cha jamii na taifa, kiwango cha mji na kupitia kwa kizazi kijacho. Katika kiwango cha kijamii na kitaifa, wanawake hawa ni chanzo

cha nguvukazi. Nguvukazi hii inatokana na wao wenyewe pamojo na kizazi chao. Pia ni msingi muhimu wa uwekaji rasilmali na kuhifadhi; aghalabu wana uwezo bora wa kutunza chochote walicho nacho kuliko wanaume. Katika kiwango cha mji, wanawake wa mashambani wanahakikisha kuwako kwa chakula, na njia za kukitayarisha chakula hicho. Katika kiwango cha vizazi, wanawake hawa wanakuwa kiungo kikubwa kati ya kizazi kijacho na vizazi vya kesho. Hawa ndio wanaowatunza, kuwalea na kuwaelimisha watoto na kuhakikisha kuwa pana muungano kati ya vizazi vya jamii.

MASWALI

i) Ni sababu zipi zinazosababisha umaskini wa wanawake wa shambani? (Maneno 50 -55)

Matayarisho

Jibu

ii) Eleza jinsi wanawake wa mashambani wanavyoathirika vibaya(maneno 40 – 45)

Matayarisho

Jibu

SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA. (ALA. 40)

a. Eleza sifa mbili za sauti|k|. **(ala.2)**

……

……

b. Andika mfano mmoja wa neno lenye muundo ufuatao: **(ala.1)**

IKII

c. Sentensi ambatano ni ipi? **(ala. 2)**

d. Unda sentensi yenye muundo ufuatao. **(ala.2)**

W+V+T+E

e. Onyesha viwakilishi (w) katika sentensi ifuatayo na ueleze ni vya aina gani. **(ala. 2)**

Wote walipewa kile kizuri.

f. Yakinisha sentensi ifuatayo. **(ala. 1)**

Hakula akashiba.

g. Kanusha sentensi ifuatayo. **(ala.2)**

Ningeenda kwake leo angenipa mawaidha.

h. Eleza dhana zinazojitokeza katika maneno yaliyopigiwa mstari. **(ala.3)**

a)Mtoto <u>mwenyewe</u> alianguka <u>mle</u>

iii) Mtoto mwenye tabia nzuri ni Yule.

i. Tunga sentensi kuonyesha vielezi vifuatavyo. **(ala.3)**

Kielezi cha wakati

Kielezi cha mahali

Kielezi cha namna/jinsi

j. Andika katika msemo halisi. **(ala. 2)**

Rafiki yetu alitujulisha kuwa tungeondoka siku iliyofuatia kuelekea Afrika kusini.

k. Unda nomino kutokana na maneneo yafuatayo. **(ala. 3)**

Neno	Nomino
3. Fikiri	_____
4. - la	
5. kubwa	

l. Tunga sentensi moja moja kuonyesha aina zifuatazo za nomino. **(ala. 2)**

i) Nomino kitenzi – jina

ii) Nomino dhahania

m. Onyesha vivumishi (v) kwa kupigia mstari na ueleze ni vya aina gani. **(ala.2)**

Waziri wa kawi anaishi katika nyumba kubwa.

n. Tumia alama ya ritifaa katika sentensi kuonyesha matumizi mawili tofauti. **(ala. 2)**

o. Bainisha viambishii katika neno lifuatalo. **(ala.3)**

Waliotutenga

p. Nyambua vitenzi vifuatavyo katika kauli ulizopewa. **(ala.6)**

Kitenzi	tendesha	tendeshea
Piga	_____	_____
-la	_____	_____
-nywa	_____	_____

q. Mahali palipotayarishwa pamejaa wageni kutoka mbali. (Anza kwa: wageni…) **(al.2)**

IV ISIMU – JAMII

Mtu X : wauza how much?

Mtu Y: Hamsini kastoma.

Mtu X: Kumbe ni expesive hivyo?

Mtu Y: Nitakupunguzia. Toa arobaini.

Mtu X: Haya. Nipatie change.

Hii ni sajili gani? **(ala.1)**

……

……

Eleza sifa tano za sajili hii. **(ala5)**

……

……

……

……

……

……

Taja athari mbili hasi za lugha ya ‘Sheng’ **(ala.2)**

……

……

……

Kwa nini vijana hutumia lugha ya ‘Sheng’ Eleza sababu mbili. **(ala.2)**

……

……

……

FORM 2 EXAMINATION TRIALS

KISWAHILI

PRACTICE TEST 5

TIME: 2 HOURS

NAME…….. ADM NO……....

SIGN……..……. DATE;…….....

Answer All the questions in the spaces provided

SEHEMU A; INSHA ALAMA 20

Andika ratiba ya siku ya wazazi shuleni

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

SEHEMU YA B: UFAHAMU: (ALAMA 15)

Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yafuatayo.

MAVAZI REKEBISHENI

Vazi njema kivaliwa, huongezeka heshima,
Staha mtu kapewa, poteendapo daima,
Mavazi duni si sawa, kina dada ninasema,
Mavazi rekebisheniusheratiumezidi.

Longi kwa nyuma kushika, na mapajani kubana,
Chupizilipowafika, dhahiri kuonekana,
Buremunaaibika, na kujishusha maana,
Mavazi rekebisheni, usheratiumezidi.

Kifuanikujikaza, maziwayaning'inie,
Kitu gani munawaza, hamna bahari nyie,
Ni ashikimwasambaza, sikizeniniwambie,
Mavazi rekebisheni, usheratiumezidi.

Msichana ni hatia, magotinikufichuka,
Hivyo basi kuvalia, rindalisoyafunika,
Huenda zusha hisia, maovuyakawafika,
Mavazi rekebisheni, usheratiumezidi.

Sitakosakuzitaja, skatimnazovaa,
Zaisha kwa mapaja, kikirikuchuchumaa,
Iko wazi nyonga moja, mkatoulivyokaa,
Mavazi rekebisheni, usheratilumezidi.

Wazi nitawasomea, nguo hizi nguo gani?
Dada zetumwakosea, kuzivaahadharani,
Ndizo hizo huchochea, usherati mitaani,
Mavazi rekebisheni, usheratiumezidi.

Nguo chini zishusheni, mwilini mzipanue,
Heri kuingia deni, za heshima mnunue,
Kuigiza za kigeni, ni utumwamtambue,
Mavazi rekebisheni, usheratiumezidi.

Betitisanamaliza, kalamunaweka chini,
Iwapo wajiuliza, nakereketwa ni nini?
Ni stahanahimiza, sio wake kuhaini,
Mavazi rekebisheni, usheratiumezidi.

MASWALI YA USHAIRI

(a) Shairi hili ni la aina gani? **(alama 2)**

……

……

(b) Eleza vina vya beti za kwanza mbili **(alama 2)**

……

……

……

(c) Toa kibwagizo cha shairi hili kisha ufafanue maana yake. **(alama 2)**

……

……

(d) Eleza maana ya misamiati hii kama ilivyotumika katika ushairi. **(alama 4)**

Staha –

Dhahiri –

Shani –

Duni –

(e) Shairi hili liko katika bahari zipi? **(alama 2)**

……

……

(f) Uhuru wa mshairiunadhihirikavipi katika shairi hili? **(Alama 3)**

……

……

……

MATUMIZI YA LUGHA (AL 30)

i) Pambanua sauti hizi kama ni ghuna au si ghuna. **(al 1)**

/Z/

/K/

ii) Eleza maana ya kiimbo. **(al 1)**

iii) Eleza maana ya shadda. **(al 1)**

iv) Eleza maana ya mofimu**.** **(al 2)**

v) Andika kwa wingi sentensi hizi. **(Al.2)**

a) Goti la mtoto liliumia.

b) Ukwato wa ngamia ni mpana.

vi) Bainisha nomino hizi ni za aina gani. **(al.2)**

i. Sukari.

ii. Mapenzi.

vii) Tumiavivumishi vya sifa katika mabanokukamilisha sentensi zifuatazo**.** **(al 2)**

1. Mtoto Yule ni _____ (nene)

2. Bei ya meli ni _____ mno (ghali)

viii) Jazapengo kwa kiulizi sahihi kisha uandike sentensi kwa wingi (al 2)

Ni mpishi _____ aliyepika.

ix) Fafanua maana ya misemo ifuatayo**.** **(al2)**

a) Kula mate.

x) Andika katika ukubwa. **(al 2)**

i) Jiji hili litapanukaupesi.

ii) Jizeelililokosa adabu limekaripiwa.

xi) Geuza sentensi zifuatazo katika hali ya usemi halisi**.** **(al 2)**

a. Ruhenialishauliwa na kasisiaache tabia mbaya.

b. Mwalimu alimwabiapremjiafanye bidii katika masomo yake.

xii) Andika vitenzi vifuatavyo katika hali ya kutendeshana. **(al 2)**

I. Penda .

II. Endesha.

xiii) Tambua kikundi nomino (KN) na kikundi tenzi (KT) katika sentensi zifuatazo. (al 2)

a) Anatembea kwa madaa kama tausi.

xiv) Kanusha sentensi zifuatazo. (Al) 2

i. Mimi nilicheza.

ii. Wewe huchora.

xv) Kamilisha methali zifuatazo **?(al 1)**

i) Cha kuvunda. _____

xvi) Andika kinyume cha maneno yafuatayo. **(al 2)**

i) Tandika _____

ii) Umba _____

xvii) Pambanua sentensi ifuatayo kwa njia ya mstari. **(al 2)**

Naimba huku nafanya kazi. _____

ISIMU JAMII(ALAMA 5)

Eleza sifa za lugha ya hotelini

……

……

……

……

……

FASIHI SIMULIZI (al 10)

1. Taja aina nne za hadithi.

……

……

……

……

2. Eleza umuhimu wa hadithi.

……

……

……

……

……

……

FORM 2 EXAMINATION TRIALS

KISWAHILI

PRACTICE TEST 6

TIME: 2 HOURS

NAME…….. ADM NO……....

SIGN……..……. DATE;…….....

Answer All the questions in the spaces provided

UFAHAMU: (ALAMA 15)

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali:

Takwimu zilizothibitishwa zaonyesha kuwa kila sekunde nane mtu mmoja hufa duniani kutokana na utumiaji wa tumbako. Kwa siku basi, watu 10,800 hufa. Wengi wa wavuta sigara huanza katika umri kati ya miaka kumi na mitatu hadi kumi na tisa. Takwimu zaonyesha kuwa mtu akivuta sigara kwa zaidi ya miaka ishirini huupunguza umri wake kwa kati ya miaka 20 hadi 25 zaidi ya ambaye hajawahi kuvuta. Hii ni kwa kuwa tumbako ina zaidi ya kemikali 4,000 zinazodhuru afya.

Mojawapo ya madhara makuu zaidi yanayosababishwa na sigara ni saratani. Kunayo saratani ya ngozi – vidonda visivyopona huchubuka ngozini na baada ya muda hugeuka na kuwa kansa. Iri ya mapafu hutokea vifuko vya hewa vinapopasuka na hivyo kutatiza uvutaji wa oksijeni na utoaji wa kabondayoksaidi. Moshi pia husababisha madhara kwa njia ya kupitisha hewa, yaani umio, ambapo njia hii yaweza hata kuzibika hivyo kulazimu tundu kutobolewa kooni ili mgonjwa aweze kupumua. Kabla ya kufika kooni na mapafuni, moshi hupitia mdomoni. Saratani ya mdomo na ulimi basi hupatikana zaidi miongoni mwa wavuta sigara. Pia kidonda chochote, kwa mfano baada ya kung'olewa jino, huwa vigumu kupona kwa mvutaji sigara.

Kwa wanawake, kuna hatari ya kupatwa na iri ya fuko la uzazi. Madhara kwenye njia nzima ya uzazi huifanya iwe vigumu kwa wanawake wavuta sigara kuhimili. Ni rahisi pia kuzaa njiti. Mtoto wa mvutaji huzaliwa akiwa mwepesi zaidi ya kawaida. Hii husababishwa na kabonimonoksaidi kutoka kwa sigara inayomdhuru mtoto tumboni. Saratani hii husababisha hata kifo cha mtoto aliye tumboni. Wengine wazaliwapo huwa na hatari ya kupatwa na saratani zaidi ya waliozaliwa na akina mama wasiovuta sigara.

Aina zaidi za saratani zinazowakumba wavuta sigara ni kama vile saratani ya pua, ya tumbo, ya figo, ya kibofu cha mkojo, ya kongosho, ya njia ya kinyesi na hata saratani ya matiti inayowaathiri zaidi wanawake.

Shida za sigara sio saratani pekee; sigara husababisha shida za macho na masikio kwa kiasi kikubwa. Mboni ya jicho yaweza kufunikwa na utando, hali inayoweza kusababisha hata upofu. Macho

yaweza kuwashwa na moshi mkali wa sigara au mishipa ya macho iathirike na kemikali zinazofika kwayo kupitia kwa mishipa mapafu yanapoathirika. Masikio nayo huathiriwa na uchafu wa tumbako unaoganda kwenye mishipa hadi sehemu za ndani za masikio. Damu hupunguza mwendo ufaao masikioni hivyo yanaugua. Moshi na kemikali za tumbako pia hujeruhi sehemu za ndani na athari hii yaweza kuenea hadi ubongoni na kusababisha utando unaofunika ubongo. Hali hizi zaweza kusababisha uziwi.

Mifupa na meno huathirika pia. Mifupa huwa myepesi, hukosa nguvu na kuwa rahisi kuvunjika. Mvuta sigara akivunjika mfupa huchukua muda wa asilimia themanini (80%) kupona zaidi ya mtu asiyevuta. Meno nayo hutatizika katika ukuaji wake kutokana na kugandwa na moshi wenye kemikali. Hali hii husababisha harufu mbaya, uchafu pamoja na kuoza kwa meno.

Ngozi ya mvuta sigara hukaushwa na kemikali kwa sahabu uwezo wake wa kujirekebisha na kujilainisha hupunguzwa pakubwa. Hali hii husababisha ukavu unaoonekana pamoja na makunyanzi yanayomfanya mvuta sigara aonekane mzee zaidi ya umri wake. Vidole navyo vilevile hugandwa na kutu ya sigara, nazo kucha na vidole hugeuka rangi vikawa vya manjano, hudhurungi au maji ya kunde. Vidole pia hukaushwa na moto na kemikali ya sigara. Nywele za mvuta sigara pia huathirika kwa kuwa kemikali huipunguza kinga ya mwili hivyo mizizi ya nywele kukosa nguvu. Nywele za mvuta sigara zaweza kung'oka mapema.

Sigara husababisha magonjwa ya moyo na vidonda vya tumbo. Kwa moyo, sigara husababisha shinikizo la damu na hatimaye mshtuko wa moyo waweza kutokea na kusababisha hata kifo. Kwa tumbo, sigara hupunguza uwezo wa kinga zake wa kuikinga dhidi ya asidi zinazosaga chakula. Pia hupunguza uwezo wa mwili wa kujikinga dhidi ya vidonda vya tumboni. Vidonda vya tumbo vya mvuta sigara huwa vigumu kupona na, ni rahisi kutokea tena baada ya kupona.

Kwa mwanamume, mpigo wa damu kwenye sehemu za uzazi huathiriwa. Hali hii ikizidi husababisha hata upungufu wa nguvu ya mbegu kwenye shahawa. Hata ugumba waweza kutokea. Pia watoto wa mwanamke mvuta sigara waweza kuzaliwa wakiwa na kasoro. Mimba zingine zilizotungwa na wanawake wavuta sigara pia hutunguka. Na si hayo tu; madhara ya sigara ni mengi zaidi.

Maswali

a) Yape makala haya kichwa. **(alama 2)**

……

……

b) Mbali na athari kwa uzazi kwa wanawake na wanaume na sura/umbo la binadamu, taja madhara mengine ya uvutaji sigara kwa binadamu. **(alama3)**

……

……

……

……

c) Kwa kurejelea kifungu onyesha kwamba sigara kwa wanawake hasa ni hatari mno. **(alama 4)**

……

……

……

……

(d) Je, ni kweli kuwa vifo vingi hutokea kwa sababu ya uvutaji sigara? Toa sababu. **(alama 2)**

……

……

(e) Eleza namna ambavyo uvutaji sigara huathiri sura ya mhusika. **(alama 3)**

……

……

……

(f) Eleza maana ya msamiati ufuatao kama ulivyotumiwa kwenye taarifa. **(alama 1)**

Gandwa _____

MATUMIZI YA LUGHA. AL 35

a) Eleza maana ya ishali zifuatazo**.** **(al 2)**

Mofimu

Viambishi

b) Andika kwa wingi sentensi hii; **(al 1)**

Goti la mtoto liliumia ————————————————————

c) Bainisha nomino hizi ni za aina gani**.** **(al 1)**

Mzee

Oduori

d) Tumia vivumishi vya sifa katika mabano kukamilisha sentensi zifuatazo. **(al 2)**

Mtoto yule ni ———————————— (nene)

Kiberiti si kifaa ———————————— kubeba. (zito)

e) Kamilisha sentensi zifuatazo kwa kuchaza viambishi vya upatanisho vya —ingine**.** **(al 2)**

Mahali ————————————————kulikobaki ni kwao.

Mwizi huyo ————————————————hakupigwa risasi.

f) Ziandike upya sentensi zifuatazo ukitumia 'O'rejeshi**.** **(al 2)**

(i) Meno ambayo yanamuuma yatatiwa dawa.

(ii) Kioo ambacho kilinunuliwa ni kipya.

g) Tambulisha vitenzi visaidizi katika sentensi hizi**.** **(al 2)**

(a) Hajaenda kusoma

(b) Niliwahi kumweleza.

h) Sahihisha sentensi zifuatazo kimapokeo. **(al 2)**

Zizi tuna sisi la ng'ombe kwetu.

Kiza cha abunuwasi kwenye kisa kinazikitisha.

i) Andika sentensi zifuatazo kwa wingi. **(al 2)**

Nitaenda alasiri kumwangalia alikoenda.

Atamwinda mnyama huyo kisirisiri.

j) Tumia kihusishi kifaacho katika sentensi zifuatazo**.** **(al 3)**

Amechuma matunda ——————rafiki yake

Walikimbia ——————swara.

Tutafanya kazi ——————wenzetu.

k) Tunga sentensi ukitumia vihisishi ukionyesha hisia zifuatazo. **(al 2)**

Furaha.

Dharau.

l) Andika kinyume cha vitenzi vifuatavyo**.** **(al 2)**

(i) Tandika

(ii) Unga

m) Kamilisha methali zifuatazo. **(al 2)**

Kawia————————————————————————————

Chovya chovya ————————————————————————

Isipowasha————————————————————————

Cha kuzama————————————————————————

n) Kanusha sentensi zifuatazo. **(al 2)**

(i) Nilimwona akicheza

(ii) Ningalienda kwake ningalimpata.

o) Tambua kikundi Nomino na kikundi Tenzi katika sentensi zifuatazo**.** **(al 2)**

Mwanafunzi amevaa sare safi mno

Sakafu ile inateleza sana

p) Andika sentensi ifuatayo katika usemi wa taarifa. **(al 2)**

"Njoo hapa" Asksri alimwita Juma.

q) Unda nomino mbili kutokana na kitenzi safari. **(al 2)**

r) Andika kitenzi kifuatacho katika kauli ya kutendeswa. **(al 1)**

Panga

FASIHI SIMULIZI AL 10

1. (a) Eleza maana ya methali **(al 2)**

……

……

(b) Fafanua sifa nne za methali **(al 8)**

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

ISIMU JAMII AL 10

✓ **(a)** Eleza maana ya sajili ya bungeni. **(al 2)**

……

……

……

(b) Taja sifa nane za sajili ya bungeni. **(al 8)**

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

FORM 2 EXAMINATION TRIALS

KISWAHILI

PRACTICE TEST 7

TIME: 2 HOURS

NAME…….. ADM NO……....

SIGN……..……. DATE;…….....

Answer All the questions in the spaces provided

ALAMA 20

1 Andika insha itakayomalizika kwa maneno haya: **"…….** siku hiyo nilirudi nyumbani nikiwa nimesikitika na kujawa na majonzi tele. Nilikuwa sijawahi kuona ajali mbaya kama hiyo"

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

B UFAHAMU (ALAMA 15)

Soma taarifa hii kisha ujibu maswali ifuatayo.

Ukandaji

Je,unajua kuwa ukandaji wa mwili umetumika kama njia mojawapo ya matibabu toka dahari? Watu wanaofahamika kutumia ukandaji kimatibabu toka jadi ni Wahindi,Wachina,Wagiriki,Warumi na Waafrika.

Ukandaji unajulikana kuwa na manufaa makubwa kimatibabu. Mathalani,ukandaji hufungua vitundu vya ngozi. Ufunguzi huu huondoa sumu mwilini kupitia kwa utoaji jasho. Pili,ukandaji hupunguza mkazo wa misuli. Misuli ikiwa na mkazo zaidi kwa muda mrefu huleta urundikaji wa asidi. Ukandaji huondoa asidi hii,huufanya mwili kuwa mlegevu,humletea mtu uchangamfu na kuondoa uchovu.

Halikadhalika,ukandaji huimarisha mzunguko wa damu mwilini kwa wepesi. Hali hii huhakikisha kuwa virutubishi vya mwili huweza kufikia viungo vyote vya mwili. Hili nalo huchangia kuzidisha uwezo wa mwili kujikinga na maradhi. Hewa safi ya oksijeni huweza pia kusambaa kote mwilini kupitia kwa uimarishaji wa mzunguko wa damu. Aidha,ukandaji wa taratibu na polepole hupunguza mkazo wa neva na kuziliwaza ukandaji wa kasi huchangamsha neva na kuimarisha utendaji kazi wake.

Ukandaji unaweza kufanyiwa kiungo chochote mwili ni. Ukandaji huu huweza kuwa na matokeo mbalimbali mwilini.

Mathalani,ukandaji wa njia ya chakula mwilini,hasa tumbo na utumbo,huimarisha usagaji wa chakula na kuchangia uondoaji wa uchafu na sumu mwilini. Nao ukandaji wa njia ya mkonjo hustawisha uondoaji wa chembechembe za sumu mwilini.

Kwa kawaida,viganja vya mikono hutumika katika ukandaji. Viungo hivi vinapaswa kuwa na wororo. Wororo huu hupatikana kwa kutumia mafuta. Mafuta ambayo ni bora zaidi kwa shughuli za ukandaji ni ya ufuta au simsim. Matumizi ya kitu chochote kama ungaunga kinachoweza kuziba vitundu vya ngozi hayapendekezwi.

Ukandaji wapaswa kutekelezwa kwa njia ifuatayo. Mtu aanzie mikono na miguu. Kisha aingie kukanda kifua,tumbo,mgongo na makalio. Hatimaye,akande uso na kichwa. Mtu anaweza kutumia kitambaa kukandia mgongo. Ni bora kutumia viganja vya mikono kukandia. Kwa njia hii,manufaa huwa maradufu. Kwanza,tutanufaika na ukandaji na wakati huo huo tutakuwa tukifanya mazoezi ya viungo. Wasioweza kujikanda,wanaweza kuomba msaada. Ni muhimu ukandaji ufuatiwe na kuoga kwa maji vuguvugu.

Kwa walio na tatizo la shinikizo au mpumuko wa damu wanaweza kubadilisha utaratibu wa ukandaji. Waanzie kichwani,kisha waelekee usoni,kifuani,tumboni,mgongoni,makalioni,miguuni na kuhitimisha mikononi.

Hata hivyo,ukandaji haupaswi kufanywa wakati mtu anaugua maradhi yoyote. Wanawake wajawazito nao wanatakiwa kuepuka ukandaji wa tumbo. Halikadhalika,ukandaji wa tumbo hauruhusiwi wakati mtu anaendesha,ana vidonda vya tumbo au uvimbe tumboni.

Hatimaye,ukandaji haupendekezwi iwapo mtu ana maradhi ya ngozi.

MASWALI

(**a)** Ukandaji ni nini? **(alama 1)**

……

……

(b) Eleza manufaa matatu ya ukandaji. **(Alama 3)**

……

……

……

(c) Ukandaji unatakiwa kutekelezwa kwa njia gani? **(alama 2)**

……

……

(d) Ukandaji unatakiwa kutekelezwa na nani na kwa nini? **(alama 2)**

……

……

(e) Onyesha ni lini ukandaji haupendekezwi. **(alama 2)**

……

……

(f) Eleza maneno yafuatayo kama yalivyotumika: **(5 alama)**

(i) ufunguzi

(ii) auni

(iii) maradufu

(iv) maji vuguvugu

(v) shinikizo la damu

(C) UFUPISHO

Soma taarifa hii kasha ujibu maswali

Kuna wataalamu siku hizi wanaosema kuwa jela si pahala pa adhabu bali pa matibabu. Yaani madhumuni ya kumtia mhalifu jela isiwe kumwadhibu kwa makosa aliyofanya bali iwe kumtibu na kujaribu kumrekebisha tabia yake ili awe raia mwema.

Zamani wahalifu waliadhibiwa kwa mujibu wa makosa waliyoyafanya. Mhalifu aliyefanya makosa madogo madogo alifungwa lakini mtu aliyeua naye aliuawa. Sasa wataalamu wanatuambia kuwa mhalifu akiadhibiwa anapokuwa kifunguno,basi akitoka hurejea tena kufanya uhalifu. Madhumuni ya kumtia jela iwe si kumwadhibu bali kumfunza tabia njema. Wanatuambia kuwa makosa afanyayo mhalifu yanatokana na matatizo ya jamii kwa jumla,nayo ni matatizo kama ya umaskini, msongamano wa watu,kosa afanyalo mhalifu si kosa lake pekee bali ni kosa la jamii nzima.

Jitu lilizoea kuua halioni kitu kumpiga mtarimbo au rungu la kichwa na kumyang'anya kila alicho nacho. Siku hizi,jitu kama hili baadhi ya wataalamu husema lisiuawe lifungwe maisha tu. Lakini 'kifungo cha maisha' ni kama tunavyokijua. Muuaji hufungwa pengine miaka kumi tu kisha husamehewa muda uliobaki. Hapo tena huwa huru ama kuifichua mali aliyoiiba na kuistarehea raha mustarehe au kurejea tena kufanya uhalifu.

Haya ni kinyume kabisa na mambo yaliyokuwa zamani. Aliyeua aliuawa kwa hivyo watu waliogopa kuua. Raia na pia askari waliokuwa wakiwasaka wahalifu walinusurika vifo kwani wahalifu wengine walichukua silaha za hatari kama bastola na bunduki.

Sasa wale wahalifu wabaya sana – mijizi, minyang'anyi na wauaji ndio wanaotukuzwa. Magazeti huwashawishi makatili hawa na kuwapa mapesa chungu nzima waeleze maisha yao ya kikatili. Magazeti haya sasa ndiyo yanayopata wasomaji wengi. Pia wachapishaji vitabu vya hadithi zinazohusikia na uhalifu, biashara zao zinazidi kustawi. Kadhalika sinema zinazoonyesha picha za ukatili; wizi na mauji hujaa watazamaji wanaoshangilia uhalifu ufanywao.

Wahalifu kwa upande mmoja wanatukuzwa na masinema vitabu na magazeti na kwa upande mwingine "haki" zao zinapiganiwa na baadhi ya wataalamu. Watu wanaowalaani wahalifu ni wale waliohasirika tu na kuteswa na wahalifu . Baadhi yao hata kulaani hawawezi kwa sababu wameshauawa,hawana tena kauli.

MASWALI

(a) Fupisha aya ya kwanza hadi ya tatu kwa maneno 50.

Matayarisho

……

……

……

……

……

……

Nakala safi (alama 6/mtiririko 2)

……

……

……

……

……

……

……

(b) Fupisha aya mbili za mwisho kwa maneno kati ya 45-50

Matayarisho

……

……

……

……

……

……

Nakala safi **(alama 6/Mtiririko 1)**

……

……

……

……

……

……

D MATUMIZI YA LUGHA: (ALAMA 40)

(a) Eleza tofauti kati ya sauti /z/ na /d/ **(ala 1)**

……

……

……

(b) Eleza tofauti kati ya:

(i) Mofimu huru

(ii) Mofimu tegemezi **(ala 2)**

(c) Ainisha viambishi katika sentensi hii.

(i) Mlipewa **(ala 2)**

(d) Onyesha kundi nomino na kundi tenzi katika sentensi hii.

(i) Nyayo za wanyama hao zimeonekana hapa. **(ala 2)**

e) Onyesha nomino za jamii katika sentensi zifuatazo

(i) Chuki baina ya jamii lazima ikomeshwe barani Afrika.

(ii) Wageni watatumbuizwa na bengi ya kayamba Afrika.

f) Bainisha vitenzi halisi kwa kuvipigia mstari

(i) Nyanchama hakufika mkutanoni

(ii) Horukut amerudi kutoka masoni **(ala 2)**

g) Eleza maana ya misemo ifuatayo.

(i) kupiga domo

(ii) kupiga kijembe **(ala 2)**

h) Tunga sentensi mbili kuonyesha tofauti kati ya maneno haya.

(i) shuka

(ii) suka **(ala 2)**

(i) Onyesha vivumishi vya sifa katika sentensi zifuatazo.

(I)(i) Anayetaka chakula kitamu ni nani?

(ii) Kiatu kirefu kimeng'oka kikanyagio.

(ala 2)

(j) Geuza neno lililopigwa mstari kuwa kiwakilishi

(i) Mtoto mbaya aliadhibiwa **(ala 1)**

(k) Yakinisha sentensi ifuatayo katika umoja.

(i) Nyuzi zisingekatika zisingepotea **(ala 2)**

(L) Tunga sentensi ukitumia viwakilishi vifuatavyo.

(i) Nafsi viambata

(II) Visisitizi

M) Tumia kiwakifishi kifuatacho kubainisha matumizi yake katika sentensi ili kutoa maana mbili tofauti.

(i) Ritifaa **(ala 4)**

N) Andika katika udogo na wingi

(i) Njusi aliyekuwa na jicho moja alianguka mtoni **(ala 2)**

(O) Taja visawe vya maneno yafuatayo.

(i) Damu

(ii) Mjinga

Q) Andika sentensi hii katika ukubwa

(i) Huyo nyoka alikatwa mkia na mvulana yule **(ala 2)**

R) Tumia kitenzi jina na kivumishi kutunga sentensi **(ala 2)**

S) Nyambua

Filisisha (tenda) **(ala 1)**

I) Sahihisha:

Kwenye nilisomea ni bali **(ala 1)**

U) Tumia herufi mwafaka kuainisha maneno katika sentensi hii.

(i) Ingawa anataka kucheza karata,ni mlevi **(ala 3)**

E. ISIMU – JAMII

Soma mazungumzo yafuatayo kisha ujibu maswali yanayofuata.

Mhudumu: Mnakaribishwa. Menyu hii hapa.
Mtakula nini?
Mteja 1: Naomba uniletee mix na ugali. Fanya haraka.
Mteja 2: Mhudumu,hebu leta madodo na chemsha mbili. Pia niletee maji ya machungwa.
Mhudumu: Sawa. Baada ya dakika moja utapata yote uliyoagiza.
Mteja 1: (Akila) Wewe-Please bring me drinking water. Yawe baridi tafadhali.
Mhudumu: Ndiyo haya hapa mezani. Glasi ndio hii pia,karibu.
Mteja 2: Nina haraka mzee. Wapi tooth pick?
Mhudumu: Hizo hapo ,mezani karibu na maji.
Mteja 1: (Akiita) Mhudumu,naomba uniletee ugali saucer tafadhali.
Mhudumu: Naam.
Mteja 2: (Akisimama) Nimeshiba. Hizi hapa pesa
Niletee change haraka niondoke.

MASWALI

a) Ni sajili gani inayohusishwa katika mazungumzo haya? **(ala 2)**

……

……

……

b) Taja sifa zozote tano za sajili hii **(ala 5)**

……

……

……

……

……

c) Dondoa msamiati unaotambulisha sajili hii **(ala 3)**

……

……

……

……

FORM 2 EXAMINATION TRIALS

KISWAHILI

PRACTICE TEST 8

TIME: 2 HOURS

NAME…….. ADM NO……....

SIGN……..……. DATE;…….....

Answer All the questions in the spaces provided

INSHA – ALAMA 20

"Wewe ni mwalimu mkuu wa shule yako. Andika hotuba utakayoitoa siku ya wazazi shuleni mwako."

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

UFAHAMU

Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali uliyoulizwa. (ala 15)

Mateso ya wanawakiwa ni suala la kijamii linalofaa kutazamwa kwa darubini kali. Hata hivyo wanoathirika zaidi ni watoto ambao bado wako katika umri unaohitaji kulelewa na kupewa mahitaji ya msingi kama mavazi, malazi, elimu na mengine anuwai. Hali ya kuachwa na wazazi imekuwa ikizikumba jamii tangu enzi za mababu na kila itokeapo, wanajamii huipokea kwa mitazamo tofautitofauti, hivyo kuwafanya wanawakiwa kuathirika sana.

Baadhi ya jamii zina imani za kijadi pamwe na mila zilizochakaa zinazozifanya kuamini kuwa baadhi ya vifo hutokana na laana. Wengine huchukulia kuwa mwendazake ameondolewa na ulogi. Imani kama hizi huifanya jamii kuwatia watoto waliochwa katika mkumbo ule ule, hivyo kuwaangalia kwa macho yasiyo ya kawaida. Hii husababisha dhana gande. Hali hii husababisha kuwachukulia watoto kama wanaotoka katika kizazi kilicholaaniwa. Jamii basi hukosa kuwapa watoto hawa stahiki yao. Hata wanapojitahidi kuiwania nafasi yao, waliowazunguka huwavunja mioyo. Jitihada zao huishia kuwa si chochote kwa kuwa jamii inawatazama kama waliolaaniwa.

Punde baada ya mzazi mmoja au wote wawili waendapo wasikorudi, inatarajiwa kwamba aliyeachiwa mtoto awe mzazi wake, mwanafamilia au jirani awajibike na kumtunza mwanamkiwa. Kunao kadha wa kadha wanaowajibika – nina wavulia kofia. Hata hivyo wengi hutelekeza jukumu hii walilopewa na Muumba. Si ajabu basi kuona kuwa idadi ya watoto wanaozurura mitaani inazidi kuongezeka kila uchao. Ukichunguza utakuta kuwa wengi wa watoto hawa ni waliopotelewa na wazazi wao. **<u>Inakera</u>** zaidi kugundua kuwa baadhi ya watoto hawa wana mzazi mmoja. Kwamba mke au mume wa mtu ameaga, au iwe kwamba mzazi mmoja alimza mtoto na kumwachia mwenzake mzigo wa ulezi, aliyeachiwa na jukumu la kumpa mwanawe mahitaji ya msingi. Machoni pa jalali, kila anayeupuuza wajibu huu ana hukumu yake siku ya kiama!

Ni haki ya kila mtoto kupata elimu. Katika katiba ya Kenya mathalan, elimu ya msingi, yaani kuanzia shule ya chekechea hadi kidato cha nne ni ya lazima. Tangu hapo hata hivyo, jamii zimekuwa zikiwanyima wanawakiwa wengi elimu. Kwamba kunao wachache wanaowaelimisha baadhi ya wanawakiwa ni kweli. Hata hivyo, wengine hukosa hata wa kuwapeleka katika shule ya chekechea, hivyo kuishia kutojua hata kuandika majina yao. Mfikirie mtu katika karne ya 21 asiyejua kusoma wala kuandika! Nani ajuaye, huenda huyo mwanamkiwa asiyepelekwa shuleni ndiye angalikuwa profesa, daktari, mwalimu, rubani au msomi mtajika na mtaalamu wa uwanja muhimu katika jamii!

Kila mtoto ana haki ya kulelewa hadi kufikia utu uzima kabla ya kupewa majukumu mazito. Katika katiba ya Kenya, utu uzima, ulio umri wa kuanza kufanya kazi huanzia miaka 18. Wanaohakikisha watoto hawa wametimiza utu uzima kabla ya kufanyizwa gange ngumu wanafaa pongezi. Hata hivyo wanawakiwa wamekuwa wakitumiwa na wengi kama punda wa huduma. Wanaaila wengine huwachukua wanawakiwa kwa machozi mengi wazazi wao waagapo na kuapa kuwahifadhi na kuwatunza wana wale wa ndugu zao, kumbe ni machozi ya simba kumlilia swara! Hata kabla ya mwili wa mzazi mhusika kuliwa na viwavi, mateso kwa mtoto yule huanza, akawa ndiye afanyaye kazi zote ngumu. Utakuta watoto wao wamekaa kama sultan bin jerehe huku

mwanamkiwa yule akiwapikia, kuwafulia nguo, kudeki, karibu hata wa waoshe miili! Kazi kama zile za shokoa huwa za sulubu na aghalabu husindikizwa kwa matusi yasiyoandikika.
Baadhi ya **waja** walionyimwa huruma huwahadaa wanawakiwa na kuwapeleka ng'ambo wakitumia vyambo, kuwa wakifika kule watapata kazi za kifahari. Maskini wale huishia kushikwa shokoa, wakawa watumwa katika nyumba za waajiri wao, bila namna ya kujinasua. Wengine huishia kutumiwa kama watumwa wa 'Kimapenzi' katika madanguro, miili yao ikawa ya kuuziwa makahaba waroho wasiojali utu. **Kujinasua** kule huwa sawa na kujitahidi kuokoa ukuni uliokwishageuka jivu, maadamu wanawakiwa aghalabu hukosa watu wenye mioyo ya huruma ya kuwashughulikia. Wengi huitumia methali ' mwana wa ndugu kirugu mjukuu mwanangwa' kuwapuuzilia mbali wanawakiwa ambao hukimbiliwa tu wabinafsi hawa wanapofaidika wenyewe.

Kipe kifungu hiki kichwa mwafaka. **(ala.1)**

……

……

Eleza dhana ya 'Mwanamkiwa. **(ala. 1)**

……

……

Ni kategoria gani ya wanawakiwa inayosumbuka sana? **(ala. 2)**

……

……

……

Taja mambo mawili ambayo baadhi ya imani na mila za jadi huchukulia kuwa chanzo cha uanaukiwa. **(ala.1)**

……

……

……

Eleza kwa kifupi hali ya elimu ya wanawakiwa. **(ala.2)**

……

……

……

Taja mateso mawili ambayo wanawakiwa wanaoahidiwa kulepekwa ng'ambo hukumbana nayo. **(ala.2)**

……

……

……

Eleza unafiki wa baadhi ya watu wa jamii ya wanawakiwa. **(ala.3)**

……

……

……

……

Eleza maana za maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika makala. **(ala.3)**

Inakela

Waja

Kujinasua

UFUPISHO

Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali uliyoulizwa

Wanawake wanaoishi katika maeneo ya mashambani katika nchi zinazoendelea ni baadhi ya watu waliotopea na kubobea kwenye umaskini mkubwa na wanaoathiriwa na matatizo kwa kiwango kikubwa ulimwenguni. Jumla ya idadi ya wanawake hawa wanaoishi chini ya kiwango cha chini cha umaskini inakadiriwa kuwa zaidi ya milioni 600. Hii ni idadi kubwa hasa ikikumbukwa kuwa ni asilimia kubwa ya wanawake wanaoishi kwenye maeneo haya.

Ulimwengu umeshuhudia ongezeko la idadi ya watu au dadiwakazi; kuwako kwa matatizo ya kiuchumi ulimwenguni; mitafaruku na vita vya kikabila, majanga ya kiasilia kama mafuriko ya maji, ukame au milipuko ya volkeno katika maeneo yanayoathiriwa nayo. Sababu nyingine ni uharibifu na ushukaji wa hali ya kimazingira, mabadiliko ya desturi au thamani za kitamaduni; kusambaratika kwa familia au misingi ya familia; utengano na hasa wakati wa shida pamoja na uhamaji wa wanaume na kuwaachia jukumu kubwa. Aidha kuna kuongezeka kwa hali ya wanawake kuwa wazazi pekee na hivyo kuongeza idadi ya miji inayoongozwa na wanawake na kukosekana kwa mikakati bora au ifaayo ya kupambana na maisha.

Wanawake wanaoishi mashambani wanaathrika vibaya sana. Kwanza, kama masikini wanaishi katika mazingira makali. Pili, kama wanawake wanakabiliana na mapendeleo ya kisera na

kitamaduni ambayo yanaudharau na kuupuuza mchango wao katika maendeleo. Tatu, kama viongozi wa miji (hasa wale wanaolea na kuzitunza jamaa zao peke yao) wanalazimika kupambana na uongozi wa miji pamoja uzalishaji. Aghalabu hawapati usaidizi au auni yoyote katika majukumu kama haya: wanalazimika kupambana nayo peke yao. Katika hali zote tatu zilizotangulia, wanawake hawapati nafasi zifaazo kushiriki katika maamuzi ya masuala yanayowahusu. Masuala mengi yanaamuliwa na wanaume bila ya kuwahusisha.

Licha ya dhiki yao kubwa, wanawake hawa wanachangia katika maendeleo ya kijamii na kiuchumi kwa njia tatu kuu. Mchango huu unaonekana katika kiwango cha jamii na taifa, kiwango cha mji na kupitia kwa kizazi kijacho. Katika kiwango cha kijamii na kitaifa, wanawake hawa ni chanzo cha nguvukazi. Nguvukazi hii inatokana na wao wenyewe pamojo na kizazi chao. Pia ni msingi muhimu wa uwekaji rasilmali na kuhifadhi; aghalabu wana uwezo bora wa kutunza chochote walicho nacho kuliko wanaume. Katika kiwango cha mji, wanawake wa mashambani wanahakikisha kuwako kwa chakula, na njia za kukitayarisha chakula hicho. Katika kiwango cha vizazi, wanawake hawa wanakuwa kiungo kikubwa kati ya kizazi kijacho na vizazi vya kesho. Hawa ndio wanaowatunza, kuwalea na kuwaelimisha watoto na kuhakikisha kuwa pana muungano kati ya vizazi vya jamii.

i) Ni sababu zipi zinazosababisha umaskini wa wanawake wa shambani? (Maneno 50 -55)

Matayarisho

Jibu

ii) Eleza jinsi wanawake wa mashambani wanavyoathirika vibaya(maneno 40 – 45)

Matayarisho

Jibu

Sarufi na matumizi ya lugha. **(ala. 40)**

Eleza sifa mbili za sauti|k|. **(ala.2)**

……

……

……

Andika mfano mmoja wa neno lenye muundo ufuatao: **(ala.1)**

IKII

Sentensi ambatano ni ipi? **(ala. 2)**

Unda sentensi yenye muundo ufuatao. **(ala.2)**

W+V+T+E

Onyesha viwakilishi (w) katika sentensi ifuatayo na ueleze ni vya aina gani**.** **(ala. 2)**

Wote walipewa kile kizuri.

……

……

Yakinisha sentensi ifuatayo. **(ala. 1)**

Hakula akashiba.

Kanusha sentensi ifuatayo. **(ala.2)**

Ningeenda kwake leo angenipa mawaidha.

Eleza dhana zinazojitokeza katika maneno yaliyopigiwa mstari. **(ala.3)**

a)Mtoto <u>mwenyewe</u> alianguka <u>mle</u>

Mtoto mwenye tabia nzuri ni Yule.

Tunga sentensi kuonyesha vielezi vifuatavyo. **(ala.3)**

Kielezi cha wakati

Kielezi cha mahali

Kielezi cha namna/jinsi

Andika katika msemo halisi. **(ala. 2)**

Rafiki yetu alitujulisha kuwa tungeondoka siku iliyofuatia kuelekea Afrika kusini.

Unda nomino kutokana na maneneo yafuatayo. **(ala. 3)**

Neno	Nomino
Fikiri	_____
- la	
kubwa	

Tunga sentensi moja moja kuonyesha aina zifuatazo za nomino. **(ala. 2)**

Nomino kitenzi – jina

Nomino dhahania

Onyesha vivumishi (v) kwa kupigia mstari na ueleze ni vya aina gani**.** **(ala.2)**

Waziri wa kawi anaishi katika nyumba kubwa.

Tumia alama ya ritifaa katika sentensi kuonyesha matumizi mawili tofauti. **(ala. 2)**

Bainisha viambishii katika neno lifuatalo. **(ala.3)**

Waliotutenga

Nyambua vitenzi vifuatavyo katika kauli ulizopewa. **(ala.6)**

Kitenzi	tendesha	tendeshea
Piga	_____	_____
-la	_____	_____
-nywa	_____	_____

Mahali palipotayarishwa pamejaa wageni kutoka mbali. (Anza kwa: wageni…) (al.2)

IV ISIMU – JAMII

Mtu X : wauza how much?

Mtu Y: Hamsini kastoma.

Mtu X: Kumbe ni expesive hivyo?

Mtu Y: Nitakupunguzia. Toa arobaini.

Mtu X: Haya. Nipatie change.

Hii ni sajili gani? **(ala.1)**

……

……

Eleza sifa tano za sajili hii. **(ala5)**

……

……

……

……

……

……

Taja athari mbili hasi za lugha ya 'Sheng' **(ala.2)**

……

……

……

Kwa nini vijana hutumia lugha ya 'Sheng' Eleza sababu mbili. **(ala.2)**

……

……

……

FORM 2 EXAMINATION TRIALS

KISWAHILI

PRACTICE TEST 9

TIME: 2 HOURS

NAME…….. ADM NO……....

SIGN……..……. DATE;…….....

Answer All the questions in the spaces provided

1. INSHA

Wewe ni mwenyekiti wa kamati ya usalama wilayani mwenu.Andaa hotuba utakayoitoa katika kikao kinachoshughulikia usalama huku ukizingatia chanzo cha tatizo hili na hatua zinazofaa kuchukuliwa kulitatua.

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

2. UFAHAMU(alama 15)

Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali yafuatayo.

Wiki iliyopita nilikuwa napanga foleni kuingia kwenye benki nilipopigwa na butwaa.Kilichonistaajabisha ni kuwa dada mmoja alikuwa aking'ang'ania kujibanza mbele pasipo kupanga foleni,bila kuwajali wateja waliokuwa mbele yake.Jambo hilo lilinikera kwani mwanamke hakuwa na wakati wa kuomba radhi kwa waliokuwa mbele yake.

Baada ya kutafakari kwa muda niliamua sitakereka wala kumlaumu kwani ni tabia iliyokita mizizi miongoni mwa wanawake humu nchini.Ni mara ngapi umewaona wanawake wakichukulia wanaume wana muda wote wa kupoteza na kuwakaripia kuwa hawawapi nafasi kwa mujibu wa msemo "ladies first"?Ni wangapi ambao huwanunia na kuwatukana wanaume kwa kuwa hawakutambuliwa wala kuwapa nafasi ya kwanza licha ya kuwa haikuwa haki yao?Ni wangapi huwaaibisha waume wao kwa kukosekana kwa hiki na kile nyumbani licha kuwa wenyewe wana uwezo wa kifedha?

Katika mahusiano wanaume wanapaswa kutambua ishara kama hizi mapema ambazo zitakutahadharisha kuingia katika uhusiano na dada ambaye katika siku zijazo hatakuthamini;ambaye kila kizuri kitakuwa chake.Bila shaka wanaume wengi watakubaliana nami kuwa sio rahisi kubaini tabia hizi miongoni mwa akina dada,kabla ya uhusiano kunoga.Halikadahlika,iwapo katika siku za kwanza za uhusiano utagundua kuwa dada ana mazoea ya kununa kwa sababu umeshindwa kutekeleza jambo fulani na kutupa matusi makali bila kuogopa,funganya virago kwani hii ni ishara atakukosea heshima siku za usoni.

Wanaume wengi hawaelewi kuwa uhusiano wa kudumu ni uwili ,kila mmoja akijitahidi kumfurahisha mwenzake .Wanajitwika jukumu la kuleta raha katika uhusiano kwa jua kwa mvua.Wamejitwika madeni ya ufukara pasi kukidhi kiu cha mwenziwe kikuacho kila uchao.Mwaunaume aingiapo matatani hutupiliwa mbali kwa madharau..Haya yananikumbusha bwana mmoja aliyeoa na kuishi na mkewe mjini .Alimtumikia kwa kila njia alipokuwa mwenye mshahara mnono.Alipofutwa kazi na mali kufifia kwa mahitaji yasiyoisha ya mkewe,mkewe alimwaibisha kwa kumfuata kila mwanaume aliyekuwa nacho na hatimaye kumtoroka kwa madai mwanamke ni kama gari.

Wanaume watakubaliana nami kuwa ni wengi wanaoishi maisha ya kunyanyaswa na wake wao bila kulalamika. Kimefika kiwango cha kupigwa,kuuawa,kutusiwa na kutishwa kupitia makundi haramu.Wengine wameendewa kwa wachawi kulainishwa wakaishia kupoteza akili zao razini.

Licha ya kishidikizo wanaume kunyenyekea na kufuatia haki za wanawake wanastahili.

Maswali

a) Eleza kilichomkera mwandishi na kwa nini? **Al 2**

……

……

b) Kutokana na taarifa hii ni ishara gani zinaashiria kuwa tabia kama hizi zimekita mizizi miongoni mwa wanawake. **Al 3**

……

……

……

c) Eleza sababu mbili zinazofaa kumfanya mwanaume kuvunja uhusiano mapema kulingana na mwandishi. **Al 2**

……

……

……

d) Eleza maana ya vifungu vifuatavyo kama vilivyotumika katika taarifa hii. **Al 3**

Kwa jua kwa mvua

Mwanamke ni kama gari

Akili zao razini

e) Wanaume wanakumbana na changamoto gani katika ndoa? **Al 3**

f) Andika neno lingine lenye maana sawa na yafuatayo kulingana na taarifa. **Al 2**

Kunoga

Pasi

iii) MATUMIZI YA LUGHA

III. Bainisha maneno katika senensi zifutazo

Mama anapika ugali **al 3**

Alifika kabla ya wote

IV. Bainisha viambishi vya neno lifuatalo. **Al 2**

Ilinyesha

V. Sahihisha sentensi hizi **al 2**

Nilimpea mkebe hizi jana.

Hizi ni zikombe za kukunywa chai.

VI. Unda vitenzi kutokana na nomino hizi. **Al 2**

Mtukufu

Mchumba

VII. Andika sentensi zifuatazo katika hali ya kutendwa **al 2**

Mzee alimwadhibu mwana kwa sababu ya utundu.

Huyu paka ndiye aliyeyanywa maziwa yote.

VIII. Kanusha sentensi zifuatazo **al 2**

Vidozo alikula wali jana akashiba.

Wavulana walicheka juzi.

IX. Eleza maana ya vitate hivi. **Al 4**

Tua

Dua

X. Yakinisha **al 2**

Wasingalisoma kwa bidii wasingalipita mtihani huo.

XI. Bainisha aina za viwakilishi katika sentensi hizi. **Al 3**

b) Yeye mwenyewe ni mwanafunzi.

c) Ambao ulipotea umepatikana.

d) Wangapi watafika?

XII. Fafanua sauti hizi./p/ na /b/ **al 2**

XIII. Eleza maana ya: **al 2**

a. Kiimbo

b. Shadda

XIV. Andika sentensi zifuatazo kulingana na maagizo

iii. Kuku alitaga yai.(hali timilifu) **al 2**

XV. Onyesha aina ya vitenzi katika sentensi ifuatyo

Leon alikuwa akicheza uwanjani. **Al 2**

XVI. Maneno yafutayo yamo katika ngeli gani? **Al 2**

b) Ugwe

c) Limau

XVII. Tunga sentensi yenye muundo ufuatao. **Al 2**

W+V+T+E

XVIII. Andika katika kinyume:

Msichana mzuri alifunga mlango. **Al 1**

iv) ISIMU JAMII (ala 10)

Soma mazungumzo yafuatayo kisha ujibu maswali yanayofuata

Mhudumu: Mnakaribishwa.Menyu hii hapa.Mtakula nini?

Mteja 1: Naomba uniletee mix na ugali.Fanya haraka

Mhudumu: Sawa mzee,Nafurahi kukuhudumia.

Mteja 2: Mhudumu,hebu leta mboga na madodo na chemsha mbili.Pia uletee maji ya machungwa.

Mhudumu: Sawa.Baada ya dakika moja utapata yote uliyoagiza.

Mteja 1: (Akila).Wewe!please bring me drinking water.Yawe baridi tafadhali.

Mhudumu: Ndiyo haya hapa mezani.Glasi nayo hii pia ,karibu.

Mteja 2: Nina haraka mzee.Wapi toothpick?

Mhudumu: Hizo hapo mezani na maji.

Mteja 1: (Akila) Mhudumu ,naomba uniletee ugali saucer tafadhali.

Mhudumu: Naam.

Mteja 2: (Akisimama)Nimeshiba.Hizi pesa.Nilitee change haraka niondoke.

Maswali

Ni sajili gani inayohusishwa katika mazungumzo haya? **Al 2**

……

……

……

Taja sifa zozote nane za sajili hii. **Al 8**

……

……

……

……

……

……

……

……

……

v) FASIHI SIMULIZI

Andika sifa nne za visasili. **Al 4**

……

……

……

……

iii) (a) Hadithi ni nini? **Al 2**

……

……

……

(b)Kwa nini hadithi hutambwa wakati wa jioni. **Al 4**

……

……

……

……

……

iv) Andika tofauti tano kati ya fasihi andishi na fasihi simulizi. **Al 10**

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

FORM 2 EXAMINATION TRIALS

KISWAHILI

PRACTICE TEST 10

TIME: 2 HOURS

NAME…….. ADM NO……....

SIGN……..……. DATE;…….....

Answer All the questions in the spaces provided

1. (INSHA) ALAMA 20

Umekutana na binamu yako aliyekuwa masomoni ng'ambo kwa muda wa miaka miwili. Andika mazungumzo kati yenu kuhusu mabadiliko yaliyotokea nchini tangu aende. **(alama 20)**

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

2. USHAIRI **(ALAMA 20)**

SOMA USHAIRI UNAOFUATA KISHA UJIBU MASWALI.

Tumeingia uwanjani, kukutana na vijana
Tahiyatuni kaeni, kusikia yenye mana,
Akili zifungueni, mpate kutulizana,
Sigara si ya kuigwa, vijana fikirieni.

Si sinema msidhani, mtaanza kuugua,
Maradhi ya vifuani, mapafu yataungua,
Sijitie ubabeni, kujitia mnajua,
Sigara si ya kuigwa, vijana fikirieni.

Mkingia shughulini, midomo itaungua,
Mtanuka midomoni, thamani kuwapungua,
Mkizitupa makaoni, hasara mtazizua,
Sigara si ya kuigwa, vijana fikirieni,

Ulevi nao acheni, twataka kuwazindua,
Mtangia hatiani, hivyo mnajizuzua,
Wengi hawawathamini, walevi wanapujua,
Ulevi msitamani, vijana fikirieni.

Usingie madawani,kalewa bila kujua,
Si bangi si heroini, siwaze kuzichukua,
Mtangia mashimoni, tubaki tukitundua,
Madawani jitengeni, vijana fikirieni.

Mkijitia uhuni, mjue mtajichubua,
Mpiga ngumi kutani, mazuri hatavumbua,
Ukimwi u mitaani, upesi utawanyakua,
Acheni kuyatamani, vijana fikirieni.

Uvivu nao acheni, utakuja wasumbua,
Vitabu kavishikeni, mazuri mtayavua,
Heshima muithamini, si watu kuwatibua,
Haki zenu zijuchi, vijana fikirieni.

Maswali:

Lipe shairi hili kichwa mwafaka**.** **(alama 2)**

……

……

……

……

Eleza umbo la shairi hili ukizingatia yafuatayo**.** **(alama 10)**

Mishororo

Vina

Beti

Mizani

Aina ya ushairi

i) Bainisha matumizi ya uhuru wa mwandishi ukizingatia: . **(alama 4)**

Inkisari

Mazda

Tafsida

e) Kufinyanga sarufi/kuboronga

……

……

……

……

j) Taja maudhui mawili kutoka shairi hili. **(alama 2)**

……

……

……

……

k) Taja tamathali moja ya lugha na mbinu ya **kisanaa** **(alama 2)**

……

……

……

3. ISIMU JAMII **(ALAMA 10)**

Taja na ueleze kaida zozote tano za matumizi ya lugha katika jamii.

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

4. **FASIHI SIMULIZI** **(ALAMA 10)**

Huku ukieleza andika sifa zozote tano za fanani/ mtambaji bora.

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

5. **SARUFI** **(ALAMA 40)**

Taja sifa mbili za kila mojawapo ya sauti hizi /s/ /z/ **(alama 2)**

……

……

……

……

Weka shadda kwenye maneno haya **(alama 2)**

Stima

Rukwama

Bainisha viambishi katika maneno **haya** **(alama 2)**

Walioandikiana

Vilivyovunjwa

Tumia kihusishi cha mahali kutunga sentensi **(alama 2)**

……

……

……

……

Eleza matumizi ya msemo huu **(alama 2)**

Pua na mdomo’

……

……

……

Eleza dhana ya ‘ni’ katika sentensi hizi. **(alama 2)**

Simameni tuombe

Ninataka tuelewane

Tumia kimilikishi cha nafsi ya tatu umoja kutunga sentensi **(alama 2)**

iv. Andika maana mbili za sentensi hii**:** **(alama 2)**

Mtoto alimlilia mama.

v. Tumia alama hizi kutungia sentensi. **(alama 2)**

Mshazari

Kistari kifupi

Andika sentensi hii bila kutumia '**amba'** **(alama 2)**

Gari ambalo lilinunuliwa jana limeibiwa.

……

……

……

vi. Nyambua vitenzi hivi katika hali ya kutendesha**.** **(alama 2)**

Oa

Kimbia

Kamilisha makundi haya**.** **(alama 2)**

Chane ya _____

Shungi la _____

Onyesha matumizi mawili ya kiambishi 'po'katika sentensi moja **.** **(alama 2)**

……

……

……

Weka maneno haya katika ngeli mwafaka**.** **(alama 2)**

Tikiti

Dole

Andika sentensi mbili sahihi kwa kurekebisha sentensi hii**.** **(alama 2)**

Huku mlimo, panawafaa watu kama nyinyi.

……

……

……

Tumia – zuri kama kielezi, kiwakilishi na kivumishi katika sentensi. **(alama 3)**

……

……

……

Kamilisha methali hii

Aso hadhari _____

Bainisha aina za maneno **(alama 2)**

Angelina ni mtoto mtukutu

Ainisha vitenzi kwenye sentensi **hii** **(alama 2)**

Yeye alishindwa kuruka kiunzi kile

Yakinisha sentensi ifuatayo**.** **(alama 2)**

Nisingemuona nisingetimiza ahadi yako

FOR THE FOLLOWING;

- ✓ ONLINE TUITION
- ✓ REVISION NOTES
- ✓ SCHEMES OF WORK
- ✓ SETBOOKS VIDEOS
- ✓ TERMLY EXAMS
- ✓ QUICK REVISION KITS
- ✓ KCSE TOPICALS
- ✓ KCSE PREMOCKS
- ✓ TOP SCHOOLS PREMOCKS
- ✓ JOINT PREMOCKS
- ✓ KCSE MOCKS
- ✓ TOP SCHOOLS MOCKS
- ✓ JOINT MOCKS
- ✓ KCSE POSTMOCKS
- ✓ TOP SCHOOLS PREDICTIONS
- ✓ KCSE PREDICTIONS
- ✓ KCSE REVEALED SETS

CALL/TEXT 0746 222 000

mwalimuconsultancy@gmail.com

THIS IS A PRODUCT OF MWALIMU CONSULTANCY

POWERED BY

MR ISABOKE

SUCCESS